

Nini matatizo ya macho ya Albino?

By SW - Melkisedeck Shine · April 15, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Mboni katika macho ya Albino haina pigmenti ya rangi. Kwa hiyo, ni rahisi macho yao kuathiriwa na mwanga. Kwani mboni ndiyo inayolinda jicho la ndani lisipatwe na mwanga mkali. Vilevile kama mboni inavyolinda jicho dhidi ya mionzi ya jua, inakuwa vigumu kuona kwa usahihi utofauti katika picha. Kwa hiyo uwezo wa kuona unatiwa mawingu mawingu. Hivyo basi, ni muhimu sana kukwepa inavyowezekana mionzi ya jua na kulinda macho kwa kuvaa miwani ya jua.

Albino mara nyingi hawaoni vizuri, na hii ina tofauti na kwa mmoja hadi mwingine. Inawezekana ni kutoona mbali, kutoona karibu au kuona mawingumawingu (ukungu). Matatizo haya hutofautiana katika Albino. Ukweli ni kuwa Albino anaweza kushiriki katika michezo mbalimbali, baadhi wanaweza kuendesha magari na wengi wanaweza kusoma maandishi ya kawaida.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25434>